**HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED GHARIB BILAL, MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KATIKA UFUNGUZI WA KONGAMANO LA MUUNGANO KATIKA UKUMBI WA HOTELI YA ZANZIBAR BEACH RESORT, ZANZIBAR APRILI 19, 2014**

**Waheshimiwa Mawaziri wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;**

**Waheshimiwa Viongozi wa Vyama vya Siasa;**

**Waheshimiwa Viongozi wa Dini;**

**Viongozi wa Serikali;**

**Ndugu Wananchi;**

**Mabibi na Mabwana.**

**Assalam Aleikum,**

**Ndugu Wananchi;**

Kwa Heshima na taadhima nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehma, kwa kutujalia uhai na siha njema na hivyo kuweza kufika hapa leo.

Kwa namna ya pekee, nitoe shukrani zangu za dhati kwa waandaaji wa kongamano hili kwa kazi kubwa mliyoifanya kwanza kwa kualika wageni mbalimbali ambao ni wawakilishi wa umma wa Watanzania ambao wamefika hapa kwa lengo la kutafakari, kujadiliana na kubadilishana mawazo kuhusu Muungano wetu na pili, kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala mbalimbali ya Muungano ambayo baadhi yetu hawayafahamu.

**Ndugu Wananchi;**
Jumamosi ya tarehe 5 mwezi huu, nilipata fursa ya kuwa mgeni rasmi katika mkutano wa hadhara ulioandaliwa na Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Mjini Magharibi uliofanyika katika Uwanja wa Kibanda Maiti. Mkutano huo ulikuwa na agenda moja kubwa, kutoa elimu ya Muungano na kufafanua kuhusu masuala muhimu ya Muungano na namna tunavyoweza kuudumisha Muungano wetu.

Katika mkutano huo tulisisitiza kwa pamoja juu ya udhati wa umuhimu wa Muungano sambamba na unyeti wa kuwa na Muungano imara usioyumba wala kuyumbishwa. Tuliufahamisha umma kuhusu masuala kadhaa na moja kubwa likiwa ni historia ya Muungano huu ambao sasa unafikia nusu karne.

Hatukumung'unya maneno katika mkutano huo katika kujibu hoja dhaifu ambazo zimekuwa zikitolewa siku za hivi karibuni, hoja zilizolenga kubeza Muungano wetu, hoja zilizolenga kudhalilisha nia ya Waasisi wetu kuamua kutuunganisha

na hoja zinazochochea hisia za kibaguzi ambazo kimsingi zinalenga kujenga chuki baina ya wananchi wa Tanzania.

Pia, tulizungumza kuhusu utashi wetu katika kuulinda na kuuenzi Muungano na tulitumia nafasi ile kutoa majibu kuhusu masuala ambayo yalionekana kutofahamika vema kwa wananchi. Eneo muhimu tulilolijadili lilikuwa juu ya mahusiano ya kijamii ndani ya Muungano sambamba na kutafakari namna ya kudumisha mahusiano haya ambayo mengi yanawahusu watu wetu kwa umoja wao.

**Ndugu Wananchi;**
Lengo la Kongamano hili ni kuendelea kuwaelimisha wananchi wetu wasio na uelewa mkubwa kuhusu Muungano na walio na kiu ya ufahamu kuhusu tulipotoka, tulipo na umuhimu wa kuendelea kuwa tulivyo kwa miaka mingine ijayo. Tena, kongamano hili linafanyika leo ikiwa zimebakia siku saba tu kufikia kilele cha miaka 50 ya Muungano wetu.

Kwanza kabisa, nitumie nafasi hii kukualikeni katika maadhimisho hayo yatakayofanyika kitaifa jijini Dar es Salaam na pili kukutakeni kutumia maadhimisho haya kuwakumbusha wenzenu walio nje ya kongamano hili kuhusu umuhimu wa siku hii katika kutunza historia yetu ili isaidie kujenga uzalendo hapa nchini.

Maadhimisho haya yanapaswa kuwa dira ya wapenda Muungano kote duniani na kuwa elimu kwa wanaobeza hatua tuliyofikia kama taifa tukiwa wamoja. Nafahamu kwamba kwa sasa kuna mjadala mkubwa kuhusu Muungano unaoendelea katika Bunge Maalum la Katiba, binafsi sitaegemea hotuba yangu kutokana na hoja hizo za Dodoma. Nitazungumza machache hapa ambayo naamini yatasaidia kongamano hili kuwa na hoja za kujadiliana.

La kwanza ni hili la kuwatakeni kutazama namna Muungano unavyoimarisha uchumi wa nchi zetu sambamba na ule wa mwananchi mmoja mmoja. Nadharia zinazosaidia kukuza uchumi katika dunia ya kwanza ni eneo la kijiografia na ya pili ni idadi ya watu. Ili bidhaa ipate soko kubwa inahitaji watumiaji na pia eneo la kuuzia bidhaa hizo.

Kwa sisi kuungana tunafanikiwa kuwa na soko kubwa na hivyo uwekezaji wa ndani na nje kuimarika. Pili, eneo letu la kijiografia linatanuka na hivyo kutoa mwanya kwa wananchi wetu kuwa na fursa kubwa ya kujipatia maendeleo.

Kazi tuliyonayo sasa ni kutafakari je, namna gani tunaweza kuendelea kutumia fursa hii tuliyonayo sasa ili isaidie wananchi wengi. Kwa mfano hapa Zanzibar tunawezaje kutanua utalii wa ndani ili uungane na ule wa nje na hivyo kunyanyua sekta hii hapa Visiwani.

**Ndugu Wananchi;**
Eneo jingine ambalo kongamano hili mnaweza kulitazama na kulitafakari, ni juu ya mahusiano yetu ya kijamii ambayo tumekuwa nayo kwa miaka hata kabla ya Muungano. Kwa mfano, mara ngapi wavuvi wamekuwa wakishirikiana wawapo

baharini katika kazi zao za uvuvi? Na mara ngapi wakutanapo na dhoruba wamesaidiana bila hata kuulizana wanakotokea? Ama fikirieni ni mara ngapi wananchi wameenda kukopa bidhaa katika maduka ya ndugu zetu Wapemba yaliyoko Bara bila kutiliana shaka?

Kama wananchi wanafikia hatua hii ya kuaminiana hata kukopeshana bidhaa je, mahusiano haya yalijengwa na nani? Bila shaka mtaona kuwa uhusiano baina ya watu wetu ni mkubwa na watu wetu wamekuwa wamoja wakishirikiana bila kujali maeneo wanayotoka!

Lakini pia, ni familia ngapi zina uhisiano wa kuoleana kati ya Bara na Visiwani? Mahusiano haya mnadhani yalihamasishwa na nini? Ni wazi kuwa majibu ya maswali haya yanaweza kuwa tofauti kati ya huyu na yule. Lakini la muhimu kuzingatia ni moja, tayari jamii zetu zimekuwa moja, zinaishi vema pamoja na kijamii hazina nongwa!

Tutafakari pia kuhusu fursa za elimu na afya ambazo zinapatikana hapa nchini. Wananchi wetu ukiwauliza kuhusu huduma hizi watakueleza kuwa kuna muingiliano mkubwa wa huduma hizi sambamba na matumizi yake. Kwa ushirikiano baina ya nchi zetu tumekuwa na elimu inayokuwa sambamba na uboreshaji wa huduma za afya. Tena, ukiyatazama masuala haya hayamo katika mambo ya Muungano lakini watu wetu wanasoma kote, wanatibiwa kote na wanafanya kazi za ufunzaji na utabibu katika maeneo yetu yote bila kuingiliwa.

**Ndugu Wananchi;**
Tatizo kubwa linalotukabili ni suala la maslahi baina ya makundi na hasa kundi la wanasiasa. Kundi hili katika Tanzania ambayo sasa ina idadi ya wananchi wapatao milioni 44 halizidi watu 2000. Kundi hili kwa miaka mingi limekuwa likitaka kuona Muungano wetu haugusi maslahi ya wananchi wa kawaida na badala yake Muungano ujikite katika masuala ya kisiasa tu. Hata sasa ambapo mjadala wa Katiba unaendelea, bado kundi hili linavutia kule kule, yaani maeneo ambayo yatanufaisha vyama vya siasa na hasa yale yatakayowawezesha kupata nafasi ya kuongoza dola.

Vipo vyama vya siasa ambavyo havina ushawishi Zanzibar. Vyama hivi lazima vitatafuta namna ya kututenga ili vipate uhalali wa kupata madaraka. Tena vipo vingine visivyo na ushawishi Tanzania Bara. Vyama hivi navyo vinafanya kazi hiyo hiyo ya kuhakikisha vinapandikiza chuki ili watu wetu watengane. Wanaamini wananchi wakitengana
Watanufaika.

Mimi ninawaambia, wanajidanganya. Dhambi ya utengano ni kubwa na watakaoathirika ni wananchi wetu ambao wananufaika sana katika faida za kijamii kuliko hizi za kisiasa.

**Ndugu Wananchi;**
Waasisi wetu wakati wakipanga kuunganisha nchi zetu walitazama sababu nyingi ambazo kwa wakati huo zilionekana zina umuhimu kwa wananchi wa nchi zetu. Moja kubwa ambayo ipo hadi sasa ni suala la usalama. Kuna baadhi yetu wanaamini kwa

kuwa Tanzania Bara ina eneo kubwa basi inahitaji kutumia gharama nyingi zaidi katika kujilinda.

Dai hili linaweza kuwa kweli lakini pia inawezekana ukawa na eneo dogo lakini gumu katika stratejia ya ulinzi. Eneo la Zanzibar kwa mfano, linapakana na bahari na humo kuna bahari ya Kimataifa inayotumika na watu wote. Kiulinzi hata gharama za kulinda eneo hili ni kubwa. Mkishirikiana inakuwa rahisi kufanikisha ulinzi wetu. Niliombe kongamano hili litambue kuwa vyote ving'aavyo si dhahabu.

Tusione tunaamka na kufanya kazi zetu na kurejea majumbani kwetu salama. Kuna watu na vyombo vinavyofanya kazi usiku na mchana ya kuhakikisha tuko salama. Watu hawa na vyombo wanavyovisimamia pia wananufaika kistratejia kutokana na sisi kuwa nchi moja iliyoungana.

Kutengana kwetu hakutaishia kutuongezea maadui wa ndani peke yake. Tutaongeza pia maadui wa nje na hivyo kutokuwa salama kabisa. Suala la usalama ni nyeti, ni suala muhimu na ni jambo gumu kulielezea kwa kila mwananchi akalielewa.

Kwa wale tulio na nafasi ya kulifahamu jambo hili tuna kila sababu ya kuendelea kulifafanua katika makongamano kama haya. Tena tunatakiwa kusisitiza juu ya umuhimu wa kusimamia Muungano kwani umeonesha kufanikisha usalama katika ukanda wetu na hata kwa nchi zinazopakana na sisi. Waswahili wanasema, 'Usione vyaelea vimeundwa!'. Kuungana kwetu kunatupunguzia maadui na kutengana kunaongeza mianya ya sisi kutokuwa salama.

**Ndugu Wananchi;**
Tunahitaji fikra yakinifu kama taifa kutafakari kwa kina kuhusu faida zinazotokana na Muungano wetu. Sina sababu ya kueleza faida za jambo hili, naamini kila Mtanzania anafahamu vizuri faida za Muungano. Hata mjadala unaoendelea sasa kuhusu suala hili, ni wazi idadi kubwa ya wachangiaji na wanaotoa maoni, wanaafiki uwepo wa Muungano, kinacholeta msigishano ni mbwembwe tu za kisiasa kuvutana juu ya aina gani ya Muungano unaohitajika.

Twende kulia au kushoto ukweli ni kwamba katika zama hizi, Watanzania tunahitaji Muungano imara kuliko kipindi chochote kile cha historia kutokana na changamoto mbalimbali za maendeleo na mabadiliko makubwa yanayoendelea kugusa kila kona ya dunia yetu hii.

Tusiongozwe na jazba tunapotafakari jambo hili na wala tusilitazame kwa kuperuzi zaidi kurasa za kasoro zake, bali tufungue vitabu vya faida zake na kuzitia nakshi kwa faida za kizazi cha sasa na kijacho cha Watanzania.

**Ndugu Wananchi;**
**Ndugu Washiriki wa Kongamano;**
Baada ya kusema hayo, kwa heshima kubwa na taadhima, sasa napenda kutamka kuwa Kongamano la Muungano limefunguliwa rasmi. Napenda niwatakie majadiliano mema yenye tija itakayosaidia kujenga mustakabali chanya kwa ustawi na maendeleo ya Taifa letu. **Ahsanteni sana kwa kunisikiliza.**